MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 2. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Oktoba 11-20, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Oktoba 21-31, 2018**

**Muhtasari**


- Kutokana na hali ya joto la bahari kuendelea kuwa juu ya wastani katika pwani ya nchi ya Somalia imepelekea mtawanyiko hafifu wa mvua za Vuli zinazoendelea katika maeneo ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hivyo wakulima wanashauriwa kufuatilia utabiri wa siku kumi kumi pamoja na kupata ushauri toka kwa maafisa ugani.
- Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri maji pamoja na malisho ya wanyama ili kukabiliana na upungufu uliopo unaosababishwa na hali ya ukavu inayoendelea kujitokeza katika maeneo mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita (dekadi), migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena naMascarene) iliendelea kudhoofika. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kubaki kaskazini lakini sehemu yake ilikaribia maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi, hivyo kusababisha mifumo ya mvua katika maeneo hayo. Pia upepo kutoka kusini mashariki uliendelea kuvuma katika maeneo ya ukanda wa pwani hususan katika siku tano za mwanzo. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani lilionekana katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha upepo wenye hewa ya unyevunyevu ingawa hakukuwa na matukio ya vimbunga. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii ilipelekea kuongezeka kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kusababisha mifumo ya mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi pamoja na ukanda wa ziwa Victoria.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, sehemu kubwa ya nchi ilikuwa kavu isipokuwa katika maeneo machache ya ziwa Victoria na mikoa ya magharibi ambayo yalipata zaidi ya milimita 50 za mvua kama inavyoonekana katika Kielelezo. Msimu wa vuli umeanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miliwi ya mvua kwa mwaka, ijapokuwa mtawanyiko wa mvua hizi bado ni hafifu katika maeneo mengi.Hali hii imetokana na joto la bahari kuendelea kuwa juu ya wastani katika pwani ya nchi ya Somalia na kupelekea unyevunyevu kuwa hafifu katika nchi yetu.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Oktoba 11-20, 2018

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 11-20, 2018

Katika kipindi cha dekadi iliyopita wakulima katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli waliendelea na uandaaji wa mashamba pamoja na upandaji, isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambapo wameanza shughuli za upaliliaji wa mazao ya mahindi na maharage. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa msimu wa kilimo unaozotarajiwa kuanza mwezi Novemba hadi Disemba. Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa si ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi, hii ni kutokana na kuwepo kwa vipindi vya ukavu.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 11-20, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu unayoendelea

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 21-31, 2018

Katika kipindi hiki**,** migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Katika kipindi cha siku tano za mwanzo migandamizo mikubwa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kidogo hivyo kupelekea kuchelewa kwa Ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kusini. Pia upepo kutoka mashariki na kaskazini mashariki unatarajiwa kuvuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi na kusababisha uwepo wa hewa yenye unyevunyevu, pia uwezekano wa kutokea kwa vimbunga baharini kwa kipindi hiki unatarajiwa hasa eneo la kusini mashariki mwa Madagascar. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupungua kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kuathiri mifumo ya mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 21-31, 2018.

Katika kipindi cha siku kumi zijazo kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) na nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe naIringa) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi kwa ujumla.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 21-31,2018

Mvua zinatarajiwa kuongezeka kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan Pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazin mashariki pamoja na kanda ya ziwa Viktoria. Wakulima wa maeneo husika wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kupanda pale kutakapokuwa na unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Hata hivyo wakulima wa maeneo ya kagera wanashauriwa kupanda mazao yanayostahimili ukame kutokana na mvua za wastani hadi chini ya wastani zinazotarajiwa. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, wakulima wanashauriwa kutozitumia mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha kwa uoteshaji wa mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa itaathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa maeneo mengi nchini hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hivyo wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OCTOBA 21-31,2018.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056: Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8: Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 : Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz: Tovuti: www.meteo.go.tz*